



TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan Trade) inayo furaha kuwafahamisha Washiriki wa Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) kuwa kutakuwa na zoezi la ushindanishwaji wa Mabanda Bora litakalofanyika tarehe 29 mpaka tarehe 30 Juni, 2017 kuanzia saa 4.00 asubuhi kwenye Uwanja wa Maonesho ya Biashara wa Mwl. J.K.Nyerere Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Washiriki watakaopenda kushindanishwa wanashauriwa kujisajili TanTrade kabla ya Maonesho hayajaanza na Washiriki watachagua kundi moja watakalotaka kushindanishwa. Vigezo vya kuchaguliwa ni kama ifuatavyo:-

- Muonekano wa jumla wa Banda la Maonesho unaovutia watembeleaji
- Muonekano wa kitaalamu wa bidhaa au huduma na mpangilio wake kwa lengo la kuvutia watembeleaji
- Kiwango na Ubora wa bidhaa na Huduma
- Uhusiano wa bidhaa na Kauli Mbiu ya Maonesho ambayo ni “Ukuzaji wa Biashara kwa Maendeleo ya Viwanda”
- Ujuzi kuhusu bidhaa au huduma unazoonesho
- Huduma kwa Wateja jinsi gani unavyopokea na kuhudumia watembeleaji

Kwa kuwa lengo la Maonesho ni kukuza biashara ya ndani na nje ya nchi, kutakuwa na tuzo kwa makundi maalum ambayo ni Mshiriki anayeonesha bidhaa bora anazouza nje ya nchi na Mshiriki anayeonesha bidhaa bora kwa ajili ya soko la ndani ili kutambua mchango wao katika soko la nje na ndani. Washiriki watakaopenda kushiriki katika makundi haya mawili wanatakiwa kujisajili TanTrade kabla ya Maonesho kuanza

Wakati wa zoezi hili Majaji hawatajitambulisha, hivyo mshiriki anatakiwa awe umeshapanga banda lake mapema. Tuzo zote zitawasilishwa katika sherehe za ufunguzi. Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu ambayo ni www.tantrade.or.tz au piga simu namba 0715988299.

Imetolewa na;

Edwin N. Rutageruka
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Juni 19, 2017